

Mafuriko na magonjwa yanayoenezwa na mbu

Habari kuhusu jinsi ya kuzuia magonjwa yatokanayo na imbu kisha mafuriko au mvua kubwa

Swahili | Kiswahili

OFFICIAL

Kisha a mafuriko au mvua nyingi, imbu hukua na kuenea katika maji isiyotingizika i yaliyoachwa nyuma. Imbu wanaweza kubeba magonjwa na kuyaeneza kwa kukuuma.

Njia bora ya kuzuia magonjwa yanayoenezwa na imbu ni kuepuka kuumwa na imbu!

Magonjwa yanayoenezwa na imbu huko Victoria ni pamoja na virusi vya Ross River, Barmah Forest Virus, Murray Valley Encephalitis (MVE) na virusi vya encephalitis ya Japani (JE). Virusi vya JE na MVE vinaweza kusababisha ugonjwa mbaya na kifo katika watu fulani. Chanjo ya JE inapatikana bila malipo kwa watu mahususi (specificiques), ongeya na daktari wako ikiwa wewe unastahili. Maelezo zaidi kuhusu chanjo ya JEV yanaweza kupatikana hapa.

Jilinde na kuumwa na imbu!

- Jufunike. Vaa nguo ndefu, zisizobana na za rangi zenye kungaa.
- Tumia dawa za kufukuza wadudu ambazo zina picaridin au DEET.
- Usisahau watoto - mda wote angalia maandishi yenye kuwa ku chupa ya dawa ya kufukuza wadudu. Kwa watoto, pulisza au paka dawa ya kufukuza imbu kwenye nguo zao pahali ya ngozi zao. Usitumie kwenye mikono ya watoto wachanga au watoto wadogo.
- Usitoke nje ikiwa unaona imbu wengi nje, hasa jioni na alfajiri (asubui mapema), ambazo ni nyakati za kuuma sana.
- Lala chini ya chandarua (moustquaire) ikiwa uko nje na hujalindwa na kaungiyoy ya wadudu.
- Tumia dawa ya kupuliza ya kufukuza inzi, mizunguko ya kufukuza imbu, au dawa ya kuingiza kwenye tundu la umeme kufukuza imbu mahali unapokusanyika ili kuketi au kula.
- Mahali ambapo kuna maji yasiyotingizika, epuka eneo hilo na ukae ndani ikiwezekana.

Kuzunguka nyumba

- Ondoa maji na vyombo ambavyo imbu huzaliana pamoja na mbegeti, mapneu ya zamani, visima vya samaki, matanki ya maji ambayo hayajazibwa na vyombo vya kuweka mimea.
- Maji katika vyombo karibu na nyumba yanapaswa kumwagwa angalau mara moja kwa wiki.
- Funika madirisha yote, milango, matundu, na viingilio vingine kwa kutumia kaungiyoy i ya wadudu.
- Ondoa uchafu au mimea iliyokomaa kwenye mifereji ya maji na mikora (majanja ya kutega maji) ya maji.
- Punguza maji katika mashimu ndani na karibu na kiwanja.
- Angalia kaungiyoy ya tanki la maji kama inafanya kazi vizuri na ubadilishe kaungiyoy zilizoharibika.

Wapi pa kupata msaada

Ikiwa una matatizo ya kiafya, muone daktari wako, au mpigie simu Muuguzi-wa-zamu (Infirmier de Garde) kwa 1300 60 60 24. Katika hali ya dharura (urgence), piga simu 000. Kwa usaidizi mwingine, tafuta baraza la mtaa (City Council) wako.

Ili kupokea chapisho hili katika muundo (format) unaofikiwa, tuma barua pepe (email) pph.communications@health.vic.gov.au

